




JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MJI NANYAMBA  
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Mji)



Simu: 0232935443  
Nukushi: 0232935442  
Baruapepe:td@[nanyambatc.go.tz](mailto:nanyambatc.go.tz)

2 Barabara ya Bomani,  
S.L.P 1490,  
63682 NANYAMBA-MTWARA

28/06/2024

## TAARIFA KWA UMMA.

### MAPOKEZI YA FEDHA KIASI CHA 1,000,184,067.41 KWAAJILI YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA ELIMU YA MSINGI NA SEKONDARI KUPITIA MIRADI YA BOOST NA SEQUIP.

Serikali Kuu kupitia Mradi wa kuboresha upatikanaji wa fursa sawa katika ujifunzaji bora wa Elimu ya Awal na Msingi Tanzania bara (**BOOST**) ambao ni sehemu ya Mpango wa Lipa kulingana na Matokeo katika Elimu awamu ya pili (**EP4RII**) unaochangia utekelezaji wa mpango wa maendeleo ya sekta ya elimu wa miaka mitano 2021/2022 mpaka 2025/2026 Pamoja na Mradi wa Uboreshaji wa elimu Sekondari kwa kila kata (**SEQUIP**) imeipatia Halmashauri ya Mji Nanyamba kiasi cha **shilingi Bilioni moja (1,000,184,067.41)** kwaajili ya ujenzi wa miundombinu ya elimu ya msingi na sekondari kwa mchanganuo ufuatao:

NA	SHULE	KATA	MRADI	KIASI
1	Shule ya Sekondari Mtimbwilimbwi	MTIMBWILIMWI	Ukamilishaji wa Bweni	26,858,044.53
2	Shule ya Sekondari Mnyawi	MILANGOMINNE	Ukamilishaji wa Bweni	63,126,022.88
3	Shule ya Msingi Likwaya	NAMTUMBUKA	Ujenzi wa matundu ya vyoo na Ukarabati	107,200,000.00
4	Shule ya Msingi Mnongodi	MNONGODI	Ujenzi wa madarasa mawili, Matundu sita ya vyoo	159,200,000.00
5	Shule ya Msingi Mwenge	KIYANGA	Ujenzi wa madarasa manne na matundu sita ya vyoo	107,200,000.00

6	Shule ya Msingi Nyundo B	NYUNDO	Ujenzi wa shule mpya yenye mkondo mmoja	334,600,000.00
7	Shule ya Msingi Nitekela	NITEKELA	Ukarabati wa shule	101,000,000.00
8	Shule ya Sekondari Mtiniko	MTINIKO	Ujenzi wa nyumba ya mtumishi	95,000,000.00
9	HALMASHAURI	Usimamizi na ufuatiliaji		6,000,000.00
		<b>JUMLA KUU</b>		<b>1,000,184,067.41</b>

Kufuatia mapokezi ya Fedha hizi, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Nanyamba kwa niaba ya wananchi na uongozi wa mzima wa Halmashauri ya Mji Nanyamba anatoa **shukrani kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhuhu Hassan na serikali yake ya awamu ya sita** kwa kudhamiria kuinua na kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia nchini.

Imetolewa Na;

**KITENGO CHA MAWASILIANO YA SERIKALI,**

**HALMASHAURI YA MJI NANYAMBA.**

